Made for minds.

# Kanuni ya Maadili

Maadili yetu. Msimamo wetu. Matendo yetu.

# Kuyaishi maadili yetu



Wapendwa Wafanyakazi Wenzangu,

DW (Deutsche Welle) huwafikia watu wengi zaidi ulimwenguni hivi sasa kuliko wakati wowote ule, ikijijengea uaminifu zaidi na heshima kama sauti huru. Tunataka kuwapa watu habari watu — hasa katika maeneo ambako utoaji habari unadhibitiwa na kutawaliwa na propaganda na kuna ukosefu wa mitizamo inayotofautiana. Hapo ndipo pia tunawakilisha misimamo yenye utata.



## Tunakuza upatikanaji wa habari bila malipo pamoja na uhuru wa kujieleza kote ulimwenguni.

Sote katika DW tuna maono sawa: wazo la uhuru, kuheshimu haki za binadamu, demokrasia na utawala wa sheria, utayari wa kupokea mawazo tofauti, uvumilivu na uwazi kwa umma. Hiyo ndiyo sababu tunakataa aina zote za ubaguzi ikiwemo ubaguzi wa kijinsia, ubaguzi wa rangi na chuki dhidi ya Wayahudi. Dhima ya kihistoria ya Ujerumani kuhusu mauaji ya Holocaust ni sababu pia kwa nini tunaunga mkono haki ya kuwepo kwa taifa la Israel. Tumejifunga kusimamia na kutekeleza maadili hayo. Hii inaakisiwa siyo tu katika maudhui za habari tunazotoa na miradi ya sera ya maendeleo na mipango ya elimu ya Chuo cha Mafunzo cha DW (DW Akademie), lakini pia katika maingiliano ya kila siku ya watu kutoka zaidi ya mataifa 160 katika utofauti wao wote.

Kama shirika la utangazaji la kimataifa linalodhaminiwa na umma, tuna wajibu maalumu kwa watumiaji, washirika wetu wa miradi, mauzo na biashara, jamii na mazingira. Kanuni hii ya Maadili inafafanua jinsi tunavyouelewa wajibu huu katika muktadha wa ndani na nje ya shirika.

Tunatekeleza kwa vitendo, maadili na kanuni, desturi na viwango tunavyowasilisha na kukuza duniani, ndani ya DW kwenyewe na kwa ushirikiano na washirika wetu. Haya yanaelezwa katika kanuni yetu ya Maadili.

Kama kanuni kuu ya maadili, inaziweka pamoja kanuni fungamanishi na viwango vya tabia vinavyoongoza matendo ya kila siku na namna tunavyohusiana. Utii wa sheria ni muhimu kwetu katika kila tunachofanya. Hivyo Kanuni ya Maadili inahakikisha tunatekeleza shughuli zetu katika mtindo wa kisheria, kwamba

tabia ya wafanyakazi wote wa DW inaendana na matakwa ya kisheria na kwamba matendo yetu yanakuwa ya kipekee kimaadili.

Kanuni zaidi za msingi ni zile za Maadili ya Uongozi wa DW, ambazo sasa zinatekelezwa katika shirika lote. Kanuni ya Maadili ni muhimu kwa kuendeleza sifa yetu na mafanikio, hapa nchini Ujerumani na kote duniani. Inanuwiwa kuwahamasisha wafanyakazi wote kutimiza malengo ya DW kwa umuhimu wa kanuni hizi pamoja na miongozo iliyopo ya ndani na kwa umuhimu wa kuziheshimu. Kanuni ya Maadili inawahusisha wafanyakazi wote wa  DW pamoja na matawi yake.

Kama wafanyakazi wa DW, sote tunawajibika kutii na kuishi kufuatana na Kanuni ya Maadili na miongozo ya kitabia iliyomo kwenye kanuni hiyo. Hii inaihusu hasa menejimenti ya shirika na watendaji ambao, kwa kiasi kikubwa, wanaunda utamaduni wa shirika. Mameneja ni watu wa mfano. Lazima wahakikishe kwamba wafanyakazi wanaijua na kuielewa Kanuni ya Maadili. Wana pia wajibu wa ziada wa kuchukuwa hatua dhidi ya tabia yoyote na zote zinazokiuka sheria zozote zilizopo au zinazoendana na miongozo au maadili ya msingi ya Kanuni ya Maadili.

Tutachunguza ukiukaji wowote wa Kanuni ya Maadili na kuchukua hatua yoyote inayohitaji kuchukuliwa, hususani katika muktadha wa sheria ya ajira. Kama shirika la utaganzaji linalotetea uhuru wa kujieleza na wa maoni duniani, tunakuza mazingira ndani ya DW ambayo yanakubali na kuvumilia upinzani halali.

Wenu,
**Peter Limbourg**
Mkurugenzi Mkuu

“Tuna maono sawa.

# Kanuni ya Maadili

Kanuni ya Maadili imeundwa kwa msingi wa, na inamaanisha sheria zote, makubaliano ya pamoja na miongozo ya ndani ya DW inayoihusu DW; na hasa zile zilizomo katika kijitabu cha DW. Bila shaka sheria hizi na miongozo ya tabia vitaendelea kutumika chini ya mwavuli wa Kanuni ya Maadili.

Kama wafanyaazi, tunatarajiwa kubeba dhima ya kujifahamisha kuhusu sheria hizi. Maswali kuhusu sheria moja moja yanaweza kuelekezwa kwa mameneja, maafisa wanaosimamia utekelezaji wa sheria na miongozo na kwa kazi husika.

# Kinachotuto-fautisha

## Taswira yetu binafsi — Taarifa zisizo na upendeleo kwa

Dhamira yetu: Kama shirika la habari la Ujerumani lisiloegemea upande wowote, tunatoa habari kwa watu ulimwenguni kote, na kuwapa uhuru wa kufanya maamuzi yao wenyewe.

Tumeundwa Kuinoa akili. Tukiwa katika mdahalo na watumiaji na washirika wetu, tunatangaza mitazamo mipya kwa msingi wa kutoa taarifa za kuaminika kwa akili pambanuzi kote ulimwenguni. Wakati huo huo, tunawapatia watu njia ya bure ya kuzifikia nyenzo za kujifunzia. Tunawasaidia kujenga maoni yao kwa uhuru na kuyaeleza pia kwa uhuru, na hivyo kuunda kwa pamoja, jamii za kidemokrasia zilizo wazi.

Haya ndiyo malengo yetu tuliyoyatangaza, lakini mkakati wetu wa kuyafikia ni muhimu pia: tuna maadili yalio wazi tunayoyahusisha na matarajio ya wazi kwa ajili yetu na kwa namna tunavyotangamana na kila moja wetu. Haya yanakwenda sambamba na yanashawishi tabia na maamuzi yetu ya kila siku.

> “Tunashirikishana mawazo na kutumia utofauti wetu kupeleka mbele mafanikio yetu ya pamoja.

### Na dhamira ya wazi kwa uhuru

Uhuru, demokrasia na haki za binadamu ndiyo misingi ya ujumbe wetu wa kiuandishi, maendeleo na wasifu. Tunatetea maadili ya uhuru na, kila tunapokuwa, tunachukua misimamo huru na ya wazi, hasa dhidi ya aina zozote za ubaguzi, ukiwemo wa kijinsia, rangi na chuki dhidi ya Uyahudi. Kutokana na historia ya Ujerumani, tuna wajibu maalumu kwa Israel.

### Mdahalo wa wazi, uliounganishwa kimataifa.

Uhalisia wa maisha ya watu na mahitaji yao ndiyo vinaongoza matendo yetu katika huduma zetu za habari na katika zile za DW Akademie. Kwa uelewa wetu mpana wa mambo, na mtandao wa kidunia na kikanda, tuko katika mdahalo na watu kutoka kote duniani. Bidhaa na huduma zetu zinatoa mtazamo mpya popote na wakati wowote zinapohitajika. Tunakuza mabadilishano yanayonuwia kujenga na unawaheshimu watu wote — wakati wote na mahali popote.

### Maarifa ya kina, mitazamo tofauti

Utofauti wetu na utaalamu ndiyo rasilimali zetu kubwa zaidi. Tunaiangalia dunia kwa shauku, tunachukua njia mpya za ujasiri, kuuliza maswali yenye mtazamo wa kukosoa na kutoa majibu huru na yaliyothibitishwa. Timu zetu za wazungumzaji wa lugha mbalimbali, nyumbani katika mataifa zaidi ya 160 ulimwenguni, kwa pamoja na watumiaji na washirika wetu, huunda maudhui za kuvutia na zenye ubora na umuhimu wa hali ya juu zaidi. Tunakuza ujenzi wa mifumo huru ya habari, tunawezesha upatikanaji wa habari, kuweka viwango vya elimu na uandishi huru wa habari. Tunashirikisha mawazo yetu na kutumia utofauti wetu kwa mafanikio yetu sote.

Maadili haya yanaunda msingi wa sheria zetu za maadili — na kuhakikisha ushirikiano wa manufaa na kuheshimiana.

# Utiifu wetu kwa sheria na kanuni

Kwa miongozo na mwenendo wake, Kanuni ya Maadili inasimamia utangamano wa jumla ndani ya DW na kuainisha mfumo wa maadili kwa ajili ya kazi zetu za kila siku. Bila shaka, sheria zilizopo na miongozo makhsusi ya kampuni vinaendelea kufanya kazi chini ya mwavuli wa Kanuni ya Maadili.

Menejiment na watendaji ndiyo mifano yetu na hivyo wana wajibu wa kuchagia utekelezaji wa Kanuni ya Maadili.

DW inategemea wafanyakazi wake kuzingatia kwa namna ya kipekee mambo yafuatayo; ambayo kuyakiuka kutakuwa na madhara katika muktadha wa sheria ya ajira.

### Marufuku ya ubaguzi kulingana na Sheria ya Jumla ya Utedendeaji wa Usawa (Allgemeined Gleichbehandlungsgesetz (AGG)).

Ubaguzi wa aina yoyote, kama vile ubaguzi wa kijinsia, ubaguzi wa rangi na chuki dhidi ya Wayahudi kwa mujibu wa AGG, hautavumiliwa, si katika shughuli zetu sisi kwa sisi, wala katika huduma zetu. Hatuwabagui wafanyakazi wowote, washirika au watu wengine ambao tunawasiliana nao katika kazi yetu, ama kwa misingi ya chuki au ubaguzi wa rangi au kwa misingi ya urithi wao wa

kikabila, jinsia, dini au mtazamo wa ulimwengu, ulemavu, umri au utambulisho kwa kingono. Tunakataa kabisa uonevu na unyanyasaji wa kijinsia. Kueneza matusi na madai yasiyo ya kweli dhidi ya watu maalum pia ni marufuku.

Hatuna uvumilivu kabisa kwa uchochezi wa chuki ya kikabila au ya rangi au tabia isiyo halali kama vile ukanushaji au udogoshaji wa mauaji ya Holocaust.

### Mipaka ya uhuru wa kujieleza

Tunafahamu kwamba uhuru wetu wa kujieleza unaisha pale unapovuka mipaka na kuwa uonevu, unyanyasaji wa kingono na tabia nyingine yoyote ya kukashifu kama vile kutoa madai ya uwongo, au kashfa.

> **“Ubaguzi hautavumiliwa, si katika shughuli zetu sisi kwa sisi tu, bali hata katika huduma zetu.**

Pia tunafahamu kwamba uhuru wa kujieleza haupo katika kukanusha au kudogosha mauaji ya Holocaust.

Kama wafanyakazi wa DW, tuna wajibu wa kuendelea kujizuwia katika maudhui na taarifa za mitandao yetu ya kijamii na machapisho mengine katika muktadha wa kitaalamu na faragha. Kizuizi hiki kinatokana na wajibu wetu kwa maadili ya DW na wajibu wetu wa kuzingatia uaminifu kwa DW kama mwajiri na kwa wafanyakazi wengine kama ilivyoainishwa katika mikataba yetu ya ajira.

Kwa kuzingatia msimamo wetu na fani yetu, tuna wajibu wa kuhakikisha, tabia zetu nje ya kazi na hadharani zinakuwa za namna ambayo hazitaathiri vibaya msimamo au maslahi ya DW. Siku zote na katika kila hali tutajiepusha kutoa aina yoyote ya maoni ya ubaguzi — ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa kijinsia, ubaguzi wa rangi na chuki. Maoni ya aina hii yanaweza kuwa na madhara kwa mujibu wa sheria ya kazi, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi.

Kama wafanyakazi, tunafahamu na kutii sheria za kimsingi, makubaliano ya pamoja, maagizo ya ndani ya DW, na hasa, kanuni zilizofafanuliwa katika kijitabu cha mwongozo cha DW ambazo ni muhimu kwa maeneo yetu ya uwajibikaji. Kanuni hizi zinaendelea kutumika na hazijabatilishwa kwa njia yoyote na Kanuni ya Maadili.

# Namna yetu ya kutangamana

## Heshima

Tunafanyakazi pamoja kwa njia ya ukweli na kuheshimiana.
Tunamuheshimu kila mtu bila kujali asili yake, jinsia, dini, ulemavu, umri au utambulisho wa jinsia.
Tunathamini maoni tofauti.
Tunaendeleza sera ya « kutovumulia katu » kuhusiana na unyanyasaji wa kingono sehemu ya kazi.
Hatutovumilia matumzi mabaya ya madaraka kwa namna yoyote ile.

## Uwazi na ushirikiano

Tunashirikisha taarifa kwa uwazi na haraka.
Tunafanya kazi pamoja kwenye maeneo, vitengo vya kibiashara na idara.
Tuko tayari kupokea mawazo mapya na ubunifu. Heshima, uwazi na ushirikiano, uaminifu, utiifu, utamaduni wa mrejesho wa manufaa pamoja na utamaduni na kazi na uongozi kulingana na malengo yetu yaliokubaliwa ndiyo misingi ya kazi yetu.

## Uaminifu

Tu wawazi na wakweli.
Tunategemewa na ni waaminifu kwa dhamira zetu.
Tunaunda mazingira ya kazi yanayowezesha mawasiliano ya wazi na mrejesho wenye msingi wa ukosoaji.

> “Tunazingatia uwazi na ukweli.

## Utamaduni wa mrejesho wa manufaa

Tunajenga utamaduni wa mrejesho wa manufaa kwa kupitia mazoea yaliyopo, tukitafuta mikakati mipya na kupitia na kutafakari juu ya mwenendo wetu.
Tunatumia makosa kama fursa ya kuboresha.
Tuna hakika kwamba watu wanaweza kubadilika na kubadilisha fikra na mawazo yao.
Tunasimamia na kutatua migogoro.
Hatuenezi madai yoyote ya uongo kuhusu wawakilishi wa DW, mameneja na wafanyakazi.

## Utiifu

Tunadumisha maadili na mikakati ya DW.
Tunashiriki kivitendo katika kuunda michakato ya mabadiliko.
Tumejifunga kwenye ukweli na uadilifu.

## Hatua za kufanikisha malengo

Tunafanya kazi kwa uhuru kutimiza malengo ya DW.
Tunatumia mawazo mapya kuhamasisha na kuhimiza ubunifu.
Tumejielekeza kwenye mafanikio.



# Maingiliano yetu na washirika na wadau wengine

### Miliki za kitaaluma

Tunaheshimu na kulinda miliki za kitaaluma za pande nyingine kulingana na sheria husika.

### Migongano ya maslahi

Tunafanya maamuzi yetu ya kibiashara kwa maslahi ya DW. Hatushawishiwi na maslahi au mahusiano binafsi.

Tunafichua uwezekano wa migongano ya kimaslahi.

Tunahakikisha kwamba washirika wetu wa biashara na miradi hawana migongano yoyote ya kimaslahi.

### Rushwa na upendeleo

Tunakataa aina yoyote ya rushwa na kuepuka hali yoyote inayoonekana kuwa ya rushwa.

Tunajizuwia na aina yoyote ya upendeleo, hongo au aina nyingine ya bakhshishi za kibinafsi.

### Washirika wa kibiashara

Tunatumia Tangazo la maadili la DW wakati wa kuchagua washirika wa kibiashara.

> “Tunafanya maamuzi yetu ya kibiashara kwa kutanguliza maslahi ya DW.

### Zawadi na bakhshishi nyingine

Tunakataa zawadi, mialiko na mapunguzo kwa wanahabari, ambayo yanautia mashakani uhuru wetu na vinavyoweza kutufanya tuchukuwe maamuzi yanayoegemea upande kuhusu masuala ya biashara.

Tunakubali zawadi nyingine, mialiko na manufaa mengine kwa uwazi kamili na kwa kufuata sheria na miongozo ya ndani.

Tunatoa zawadi na mialiko ndani ya mipaka inayokubalika tu. Suala la kipi kinafaa linategemea kimsingi mtazamo wa Ujerumani, lakini pia tunazingatia mtazamo wa nchi inayolengwa.

### Ununuzi na zabuni

Tunanunua bidhaa, huduma na vipindi kwa kuzingatia ubora, uchumi na ushindani kulingana na sheria zinazohusika na kanuni za shirika. Maamuzi ya ununuzi yanategemea uhakiki wa ubora wa bidhaa na huduma za muuzaji. Makubaliano yanayoharibu ushindani hayaruhusiwi.

# Jinsi tunavyoshughulikia taarifa

## Usiri

Tunashughulikia siri za kibiashara na taarifa za siri kwa uangalifu. Hii inahusu maudhui ya habari pamoja na taarifa nyingine zisizopaswa au zisizonuwiwa kuwekwa hadharani.
Tunatoa taarifa za siri, hata kama zipo kwa mfumo wa kidijitali, kwa wafanyakazi wanaozihitaji tu.



## Ulinzi wa data

Tunakusanya data zinazohitajika tu (uchumi wa data).

Tunahakikisha kwamba tunadumisha usiri wa hali ya juu tunapokusanya, kutumia na kuchakata data za mtu binafsi na tunafanya haya; ikiwa tu sheria inaruhusu, na hivyo basi kulinda data hizo kutokana na matumizi mabaya.

Tunazingatia usiri tunapotaka kuamua mahali pa kuhifadhi data hizo na tunazingatia usiri tena tunapotaka kuamua ikiwa tutaificha kidijitali au la.

## TEHAMA na usalama wa taarifa

Tunapofanya kazi na mifumo ya TEHAMA, tunazingatia sheria na kanuni za TEHAMA na usalama wa habari ili kuzuia utumiaji mbaya wa mifumo hii, ndani ya shirikai na nje ya shirika.

Tunafahamu vitisho kwa usalama wa taarifa za DW vinavyoweza kutokana na utumiaji mbaya wa mifumo ya TEHAMA na tunachukua hatua kwa kuzingatia hayo.



“Tunashughulikia data kwa uangalifu.

# Mawasiliano yetu na umma




> “Tunabainisha wazi iwapo tunatenda au **kufanya kazi kama watu binafsi au kama wafanyakazi wa DW.**

Hatujibu binafsi maswali kutoka kwa wanahabari na makampuni ya habari kuhusu DW kwa ujumla, lakini tunayawasilisha kwa idara yetu ya mawasiliano inayoratibu na kusimamia mtiririko wa mawasiliano.

Katika mawasiliano yote, tunabainisha wazi iwapo tunatenda kama watu binafsi au kama wafanyakazi wa DW.

Ili kuepusha uwezekano wa migongano ya kimaslahi, tunashiriki tu shughuli za nje zinazoweza kuwa na athari chanya ya utangazaji kupitia utaratibu wa ndani wa uidhinishaji.

# Viwango vyetu vya **usalama na uendelezaji**




“Tunafanyakazi kwa njia endelevu.

Tunatekeleza miongozo ya afya na usalama kazini.

Tunafuata miongozo yetu ya kupeleka watu kwenye maeneo ya mizozo.

Tunatenda katika namna endelevu, hasa kwa kutumia rasilimali zilizopo na kuhakikisha urejeleaji.

Tunahakikisha kwamba matendo yetu hayana athari hasi kwa washirika wetu (Hayadhuru).



# Jinsi tunavyoshughulikia mali ya kampuni

Tunatumia vifaa vyetu vya kikazi na mali nyingine za DW kwa uangalifu mkubwa.

Tunawasilisha matokeo ya kazi zetu kwa DW.

Tunapotumia vifaa vya kazi, tunavitumia vizuri na kwa ufanisi.



“Tunazingatia ufanisi na uchumi.


Made for minds.

# Kanuni na viwango vyetu vya uhariri

Tunafahamu jukumu tulilo nalo kwa umma kama washawishi wa maoni na tunazingatia hilo.

Tunatekeleza majukumu yetu kwa mujibu wa sheria ya DW na Kanuni ya Maadili.

Tunafanya kazi yetu kwa uhuru bila kushawishiwa na maslahi ya watu wa nje.

Tunaheshimu maoni tofauti kuhusiana na wingi na utofauti wa mitazamo na kukuza mjadala.

Tunazingatia kanuni ya umakini wa kiuandishi, kufanya utafiti wa kina na kuripoti kwa ufahamu na bila kuegemea upande.

Tunaheshimu sheria zinazoongoza utenganishaji wa maudhui za matangazo na habari.

Tumejifunga kuheshimu faragha na ushughulikiaji sahihi wa habari, maoni na picha.

Tunaheshimu miongozo ya mitandao ya kijamii ya DW na miongozo ya kiuandishi ya Mhariri Mkuu.



“Tunaheshimu kanuni za uchunguzi yakinifu wa kiuandishi.



# Miongozo ya utekelezaji wa Kanuni ya Maadili

## Madhara ya ukiukaji wa Kanuni ya Maadili ya DW

Unapotokea ukiukaji wa Kanuni ya Maadili, DW itachukua hatua kufafanua na kuzuia kujirudia kwa matukio sawa na hayo katika siku zijazo. Kwanza, hatua hizi zitahusisha majadiliano na mfanyakazi husika kueleza umuhimu wa Kanuni ya Maadili kwa lengo la kuleta mabadiliko katika tabia ya mtu huyo kuhusiana na kanuni iliyokiukwa. Uzito wa kosa utafafanua ni hatua gani zinazohusiana na sheria ya kazi zinahitajika na zinazofaa. Ikibidi, hizi zinaweza hata kujumuisha usitishaji usio wa kawaida wa uhusiano wa ajira au huduma.

## Maswali yafuatayo yanaweza kukusaidia kutekeleza Kanuni ya Maadili

Je, ninafuata miongozo ya shirika na ya kisheria?
Nimemhusisha mhusika yeyote mwingine katika uamuzi, mapema na kwa wakati?
Ninafanya uamuzi wangu kwa maslahi ya DW pekee, bila kuingiza maslahi yangu?
Ni ipi athari ya nje ya uamuzi wangu? Uamuzi huo unaweza kutathminiwa na upande wa nje? Je, sifa nzuri ya DW itabaki kufuatia uamuzi wangu?
Naweza kupatanisha uamuzi wangu na dhamiri yangu?

Ikiwa unaweza kujibu maswali hayo kwa “Ndiyo” ya wazi, basi uamuzi wako unapaswa kuendana na matakwa ya Kanuni ya Maadili. Lakini ikiwa huna uhakika, watu wafuatao wanaweza kukusaidia.

# Watu wetu wa kuwasiliana nao kwa maswali yoyote



**Ikiwa huna uhakika au una maswali yoyote kuhusu utekelezaji Kanuni ya Maadili, tafadhali wasiliana na wasimamizi wako wakuu au afisa anayesimamia masuala ya kisheria.**



## Watu wetu wa kuwasiliana nao ikitokea ukiukaji

Kanuni ya Maadili ni seti ya sheria zinazowalazimu wafanyakazi wote wa DW.

Ukibaini ukiukaji wowote katika shirika letu, ni muhimu kwanza kuzungumza moja kwa moja na mtu unayedhani anatenda sivyo. Tafadhali wasiliana nasi ikiwa wewe mwenyewe umeshuhudia ukiukaji wa Kanuni ya Maadili.

Kutegemea na aina ya ukiukaji, unaweza pia kuripoti tukio hilo kwa meneja wako au afisa wa utekelezaji Annelie Gröniger:
**annelie.groeniger@dw.com**
**+49.228.429-2105**

Bila shaka, unaweza pia kuwasiliana na wahusika wengine, hasa wawakilishi wa wafanyakazi au, ikihitajika, afisa wa nje wa kupambana na rushwa au watu wenye jukumu la ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa kingono.

Katika hali yoyote, unaweza kuwa na uhakika kwamba ripoti yako itashughulikiwa kwa usiri wa hali ya juu.

## Hatua zinazochukuliwa na DW pale ukiukaji unapotokea

Inapotokea ukiukaji, DW itachukua hatua stahiki kwa ufafanuzi. Hatua hizi zinahusisha mazungumzo na mfanyakazi husika kufafanua umuhimu wa Kanuni ya Maadili kwa lengo la kuleta mabadiliko katika tabia ya mhusika kuhusiana na sheria zilizomo. Hata hivyo inawezekana kwamba ukiukaji huo utapelekea hatua ndani ya mfumo wa miongozo husika na kwa mujibu wa sheria za kazi.

Kufikia Novemba 2022 | © DW